JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

SEMINA ELEKEZI KWA VIONGOZI NA WATENDAJI WAKUU WA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA – NGURUDOTO MOUNTAI LODGE ARUSHA 13-18/MACHI 2006.

SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA NA.8 YA MWAKA 2002 NA MAJUKUMU YA TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Imetolewa na:-
Bibi Thecla W. Shangali,
Katibu,
Tume ya Utumishi wa Umma,
S. L. P. 9143,
DAR ES SALAAM.

MACHI, 2006

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Utumishi wa Umma imeundwa chini ya Kifungu Na.9 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002. Tume ni chombo huru cha Serikali cha usimamizi wa utumishi wa umma na kipo chini ya Ofisi ya Rais na ilianza kufanya kazi rasmi tarehe 7/01/2004 baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya uteuzi wa Mwenyekiti, Makamishna, Katibu na Manaibu Katibu wa Tume.

Tume ina wajibu wa kuhakikisha kuwa utumishi wa umma ni mmoja na kuwa watumishi wote wana taratibu za usimamizi, hadhi, haki na maslahi yanayofanana. Hivyo, kazi kubwa ya Tume ni kuhakikisha kuwa masuala ya Utumishi yanaendeshwa kwa haki na usawa na yanalenga katika utendaji wenye malengo maalum.

Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 imefuta Sheria zilizounda Tume zifuatazo:-

- Tume ya Utumishi wa Serikali za Mitaa iliyoundwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1982.
- Tume ya Utumishi wa Walimu iliyoundwa kwa Sheria Na.1 ya mwaka 1989.
- Tume ya Utumishi Serikalini iliyoundwa kwa Sheria Na.16 ya mwaka 1989.

Lengo la mada hii ni kujadili **Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002, Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma**, **changamoto** na **matarajio ya Tume**.

2.0 MUUNDO WA TUME

2.1 Wajumbe wa Tume

Kwa mujibu wa kifungu Na.9(1), cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kikisomwa pamoja na Kifungu 14(1)Tume inaundwa na Mwenyekiti na Wajumbe wasiozidi sita (6) na Katibu wa Tume ambao wote huteuliwa na Rais.

2.2 Idara za Tume

Kwa mujibu wa Sheria Na.8 ya mwaka 2002, kifungu Na.15(1) Tume imegawanyika katika Idara tano (5) ambazo ni:-

- Idara ya Utumishi Serikalini
- Idara ya Utumishi wa Walimu.
- Idara ya Utumishi wa Serikali za Mitaa.
- Idara ya Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji.
- Idara ya Utumishi wa Afya.

Idara hizi zinaongozwa na Manaibu Katibu wa Tume. (Ona Kiambatisho “A”). Aidha, ipo pia Idara ya Utawala na Utumishi ambayo inashughulikia masuala ya utumishi ndani ya Tume. Ona Kiambatisho “A”.

3.0 MADHUMUNI YA KUUNDWA KWA TUME

Tume iliundwa ili kuweza kutekeleza Programu ya Uboreshaji wa Utumishi wa Umma na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, ya mwaka 1999 baada ya Serikali kubaini upungufu katika utoaji wa huduma uliokuwepo wa vyombo vya Serikali kwa Umma.

Upungufu huo ulitokana na:-

- Kushuka kwa tija na ari ya utumishi.
- Mmomonyoko wa maadili ya kazi.
- Kutokufuatwa kwa Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi.
- Udhibiti hafifu wa watendaji.
- Kukithiri kwa vitendo vya rushwa.
- Kutokuzingatia sifa na uwezo katika ajira, uteuzi na upandishwaji vyeo wa Watumishi wa Umma.
- Kutokuwa na viwango maalum vya vigezo vya kubaini nafasi za kazi zilizo wazi.
- Kutokufuatwa kwa taratibu za kiutumishi katika kufanya maamuzi mbalimbali kama vile uhamisho wa watumishi na upandishwaji vyeo, hali iliyotoa mianya ya rushwa na utoaji huduma kwa upendeleo.
- Upandishwaji vyeo kwa kuzingatia muda wa utumishi kazini na uzoefu kazini bila kujali tija ya mtumishi husika.
- Usiri mkubwa katika kupima utendaji kazi wa watumishi.
- Kutokuwa na uwiano wa watumishi katika Idara mbalimbali za Serikali, hali iliyosababisha baadhi ya maeneo kuwa na mlundikano wa watumishi na maeneo mengine kuwa na upungufu mkubwa wa watumishi au kazi moja kuwa na watumishi wengi.
- Viwango vidogo vya mishahara isiyolingana na gharama halisi ya maisha.

4.0 MAJUKUMU YA TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Tume iliundwa na kupewa majukumu kwa mujibu wa kifungu cha (10) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002.

Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kumshauri Rais kupitia Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yake aliyopewa kikatiba chini ya Ibara ya 36 kuhusu ujazaji wa nafasi zilizo wazi katika Utumishi wa Umma kama Rais atakavyohitaji.

(b) Kumsaidia Rais kuhusu masuala ya Utumishi kama atakavyohitaji.

(c) Kutoa miongozo, kufuatilia na kuhoji taratibu zilizotumika na mamlaka za ajira katika kutekeleza kazi za ajira na uthibitishwaji kazini, ili kuhakikisha kuwa misingi ya uwazi na sifa imezingatiwa kikamilifu

(d) Kuwezesha uteuzi na ajira za nafasi mbalimbali katika Utumishi wa Umma

(e) Kuwezesha, kufuatilia na kutathimini utendaji kazi wa watumishi wa Umma wa ngazi mbalimbali ili uwe na ufanisi na unaowajali wateja na wenye kuzingatia matokeo.

(f) Kusimamia na kufuatilia uzingatiaji wa kanuni na maadili katika utendaji kazi wa viongozi wa Utumishi wa Umma hususan katika maeneo ya mafunzo, ajira, upandishwaji vyeo na mashtaka ya nidhamu ya watumishi.

(g) Kupokea na kushughulikia rufaa kutoka kwa watumishi na Mamlaka mbali mbali za Nidhamu katika Utumishi wa Umma.

(h) Kuwaita na kupata maelezo kutoka kwa viongozi na watendaji pale inapokuwa na ushahidi au malalamiko yanayoonesha usimamizi au utendaji usioridhisha kinyume cha shabaha na madhumuni ya Utumishi wa Umma.

(i) Kuhakikisha kuwa taratibu za uendeshaji katika Utumishi wa Umma za makundi mbalimbali ya Utumishi zinatungwa na kutekelezwa ipasavyo.

(j) Kuwachukulia hatua kupitia kwa mamlaka zao za nidhamu viongozi na watendaji watakaoshindwa kuwashughulikia watumishi walio chini yao kwa mujibu wa Kanuni na taratibu zinazosimamia utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.

(k) Kutekeleza majukumu kama yalivyoainishwa kwenye Sheria hii na Sheria nyinginezo.

Aidha kifungu cha 16 cha sheria Na.8 ya mwaka 2002 kinaitaka Tume ya Utumishi wa Umma kuwasilisha taarifa ya mwaka kuhusu hali ya Utumishi wa Umma kwa Rais.

5.0 MAMLAKA ZA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

5.1 Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 inawapa Watendaji Wakuu Serikalini na Mamlaka za Serikali za Mitaa, mamlaka ya kuajiri, kuthibitisha kazini na kupandisha vyeo watumishi walio chini yao.

5.2 **Rais** – Ndiye mwenye mamlaka ya juu kabisa katika utumishi wa umma na ndiye mwenye mamlaka ya uteuzi wa Viongozi Wakuu Serikalini na Wakurugenzi wa Majiji.

5.3 **Katibu Mkuu Kiongozi** ni Mamlaka ya kuwathibitisha kazini Watendaji Wakuu wote wenye uteuzi wa Rais.

5.4 **Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa** ni Mamlaka ya Ajira na kuthibitishwa kazini kwa Wakurugenzi wa Halmashauri isipokuwa Wakurugenzi wa Majiji.

5.5 **Makatibu Wakuu wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Makatibu Tawala Mkoa, Kamishna wa Huduma za Zimamoto na Uokoaji, Mkurugenzi wa Uhamiaji na Mamlaka za Serikali za Mitaa** ni Mamlaka za ajira, kuthibitisha kazini, kupandisha vyeo kwa watumishi walio chini yao isipokuwa wale walioteuliwa na Rais na wale ambao Mamlaka ya Ajira ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

5.6 Idara ya Utumishi wa Walimu ni Mamlaka ya Ajira, kuthibitisha kazini, kupandisha vyeo walimu wote walioko katika Utumishi wa Umma.

6.0. UTEKELEZAJI WA MASUALA YA AJIRA .

Taratibu za Ajira zina lengo la kujenga utumishi wa umma wenye Uwezo, ujuzi na taaluma husika. Kwa maana hiyo, ajira sasa inapaswa kuzingatia sifa na ushindani. Katika kutekeleza majukumu ya ajira, kuthibitishwa na kupandishwa vyeo watumishi katika Utumishi wa Umma, Mamlaka za Ajira zinatumia vyombo vifuatavyo:-

a) **Bodi za Ajira** - kwa watumishi wa Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Kanuni ya 127 hadi 144 ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Umma za mwaka 2003;

b) **Kamati maalumu za Ajira** – kwa watumishi wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji na Sekretarieti za Mikoa, kama ilivyoanishwa kwenye Kanuni 9(3);

c) **Kamati za Mikoa na Wilaya kwa ajili ya Walimu** - Kamati hizi zimeundwa na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Kifungu 29 (2) (b) cha Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 kikisomwa pamoja na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, Kanuni ya 113 – 115 na Kanuni 120.

6.1 Majukumu ya Bodi za Ajira, Kamati Maalum za Ajira, na Kamati za Ajira Mikoa na Wilaya:

6.1.1 Majukumu ya Kamati Maalum za Ajira

Taratibu za kuajiri mtumishi zimeanishwa kwenye Kanuni na 9 hadi 13, za Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Majukumu ya Kamati kwa ujumla ni pamoja na kufanya Usaili na kuwasilisha majina ya wasailiwa kwa Mamlaka ya Ajira ambayo itaajiri mtumishi/watumishi miongoni mwa waombaji waliofaulu usaili baada ya kushauriana na Kiongozi wao sehemu ya kazi. Muundo na majukumu ya Kamati maalum za Ajira yamefafanuliwa zaidi kwenye Mwongozo wa Tume Toleo Na. 1, mwaka 2004, Nyongeza Na.2

6.1.2 Bodi za Ajira

Taratibu za kuajiri watumishi walio katika Utumishi wa Serikali za Mitaa umeelezwa

kwenye Kanuni 127 hadi 144, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Majukumu ya Bodi za Ajira ni kufanya usaili, na kuwasilisha majina ya waliosailiwa kulingana na kufaulu kwao kwa mamlaka ya Ajira, ambayo itaajiri Mtumishi/Watumishi miongoni mwa waombaji waliofaulu usaili.

Muundo na Majukumu ya Bodi za Ajira yamefafanuliwa na Mwongozo wa Tume Toleo Na. 1 ya mwaka 2004, nyongeza Na. 1.

6.1.3 Kamati za Ajira za Mikoa na Wilaya

Idara ya Utumishi wa Walimu katika Tume ya Utumishi wa Umma, itakuwa na Kamati za Ajira zitakazokuwa zinashughulikia masuala ya Ajira kwa watumishi walio kwenye Utumishi wa Walimu, kama ilivyoainishwa kwenye Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 Kifungu 29 (3), Kanuni 113, Kanuni 114, na 120 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003.

Muundo na Majukumu ya Kamati za ajira yamefafanuliwa na Mwongozo wa Tume, Toleo la 1, mwaka 2004, Nyongeza Na. 3.

6.2 WAJIBU WA KAMATI ZA AJIRA

Katibu wa Kamati au Bodi za Ajira anawajibu wa kufanya Mambo yafuatayo:-

- Kutayarisha makabrasha yenye taarifa muhimu zifuatazo:-

- Kibali cha Ajira
- Vacancy form GD 3B
- Person specification
- Job description
- Tangazo la kazi.
- Kuandaa vikao vya Kamati na Bodi za Ajira.
- Kutayarisha maswali yatakayopitiwa na Kamati na Bodi za Ajira.
- Kutayarisha utaratibu utakaotumika katika usaili
- Kutayarisha orodha ya waombaji watakao fanya usaili .
- Baada ya usaili, kuandaa mapendekekezo ya Kamati na Bodi za Ajira na kuziwasilisha kwa mamlaka ya Ajira husika.
- Kuandaa orodha ya kuwathibitisha watumishi kazini na kuwasilisha kwenye kamati na Bodi za Ajira.
- Kuandaa orodha ya kuwapandisha vyeo watumishi itakayowasilishwa kwenye Kamati na Bodi za Ajira.
- Kutunza kumbukumbu za mikutano ya Kamati na Bodi za Ajira.

Mwongozo wa utaratibu wa kuendesha usaili umefafanuliwa kwenye Mwongozo wa Tume Toleo Na. 1 Mwaka 2004, Nyongeza 5.

7.0 MAMLAKA YA TUME KWA MAMLAKA MBALIMBALI ZA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Katika kutekeleza masuala ya ajira katika utumishi wa Umma, Mamlaka za ajira zinapaswa kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma pamoja na miongozo na nyaraka mbalimbali zinazotolewa na Serikali. Ili kuhakikisha kwamba maelekezo hayo ya Serikali yanatekelezwa, Tume imepewa mamlaka kisheria kwa mujibu wa kifungu Na. 10 (c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya 2002 kusimamia na kufanya ukaguzi kwa mamlaka za ajira, kuhakikisha kuwa ajira katika Utumishi wa Umma zinazingatia sifa na ushindani. Katika kuhakikisha kuwa hili limetendeka kibali cha Ajira kinapotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mamlaka za Ajira zinapaswa kuzingatia yafuatayo:-

- Kutangaza nafasi za kazi katika magazeti yanayosomwa kitaifa na kimaeneo angalau matoleo mawili.
- Kupokea barua za maombi na kuorodhesha waombaji wote.
- Kufupisha orodha ya waombaji kwa kuzingatia sifa.
- Kuita orodha ya waombaji waliofupishwa kwenye usaili.
- Kutumia Bodi za Ajira, Kamati Maalum za Ajira na Kamati za mkoa na Wilaya katika kuendesha usaili.
- Kuhakikisha nafasi moja inashindaniwa na watu watatu.
- Kuhakikisha wasailiwa wote wanahojiwa na Bodi au Kamati Maalum za Ajira zenye Akidi isiyopungua nusu ya wajumbe.

- Kuzingatia sera ya Menejimenti ya Ajira inayosisitiza upendeleo wa wanawake endapo msailiwa wa kike na wa kiume wamelingana.
- Kutoa kipaumbele kwa walemavu kwa kuzingatia Sheria ya Ajira kwa walemavu Na.1 ya mwaka 1982.

8.0MAPUNGUFU YALIYOJITOKEZA KATIKA MCHAKATO WA KUSHUGHULIKIA AJIRA

Katika mchakato wa ujazaji wa nafasi zilizo wazi kwa kutumia Kamati Maalum za Ajira, Bodi za Ajira na Kamati za Mikoa na Wilaya. Tume iligundua ukiukwaji wa taratibu za ajira kama ifuatavyo:-

- Kuitwa kwenye usaili watu wasio na sifa.
- Kusaili watu ambao hawajaomba nafasi hizo.
- Kuteuliwa mtu ambaye hakuomba cheo wala hajafanya usaili.
- Kutoandaliwa maswali maalum ya usaili hivyo kusababisha kutokuwepo na usawa katika kutoa alama kwa wasailiwa.
- Kutumia kura badala ya kutoa alama kwa kuzingatia matokeo ya usaili.
- Kuendesha usaili bila kibali cha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma au kutumia kibali ambacho muda wake umepita.

9.0 MAMLAKA ZA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma zimeainishwa katika kifungu cha Sheria 4 (1) (d), na 6 (1) b, 6(6) na Kanuni 35 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za

mwaka 2003, na Aya ya 7, na 12 (b) cha Taratibu za uendeshaji za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Mamlaka hizo ni kama ifuatavyo:-

- **Katibu Mkuu Kiongozi:**

  Ni Mamlaka ya Nidhamu kwa Watumishi wote wanaoteuliwa na Rais.

- **Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa:**

  Ni Mamlaka ya nidhamu kwa Wakurugenzi wa Halmashauri za mitaa.(kifungu cha 5(i)(a)(iii) cha Sheria ya Utumishi na kanuni Na.35(2)(b).

- **Watendaji Wakuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

  Ni Mamlaka ya Nidhamu kwa Watumishi wote ambao mamlaka ya ajira ni Watendaji Wakuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

- **Wakuu wa Idara na Sehemu**

  Ni Mamlaka ya nidhamu kwa watumishi walio kwenye masharti ya kawaida.

- **Idara ya Utumishi wa Walimu**

  Ni mamlaka ya nidhamu kwa walimu walio katika utumishi wa Umma.

9.1Taratibu za kushughulikia masuala ya Nidhamu

Ili haki ionekane inatendeka kwa mwajiri na kwa mwajiriwa, ni muhimu Mamlaka za Nidhamu zikafuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo:-

Mtumishi wa Umma hataweza kufukuzwa au kuachishwa kazi mpaka:-

- Amefunguliwa mashtaka rasmi ya nidhamu.
- Amepewa muda wa kutosha wa kujitetea/kujieleza
- Uchunguzi katika tuhuma umefanywa.

10.0 MAMLAKA YA TUME KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA UMMA:

Ili kuhakikisha kwamba mamlaka mbalimbali za nidhamu zinatenda haki katika kushughulikia masuala ya nidhamu, Tume ya Utumishi wa Umma imepewa mamlaka kwa Kifungu Na. 10(1)(C) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kukagua na kuangalia kama mamlaka za nidhamu zimeshughulikia masuala ya nidhamu kwa kuzingatia haki na kufuata taratibu. Kwa misingi hiyo, Tume itakuwa inakagua kama zimefuata haki na taratibu kwa kuangalia hatua zifuatazo:-

- Mtuhumiwa amepewa Hati ya Mashtaka ikiwa na maelezo ya mashtaka na amepewa notisi ya mashtaka.
- Mtuhumiwa amepewa nafasi ya kutoa utetezi.
- Kamati ya Uchunguzi iliyoundwa ina sifa zilizotajwa, imefuata hadidu za rejea na haikupendekeza adhabu.
- Barua ya adhabu imeonyesha makosa aliyotiwa hatiani na Haki ya kukata Rufaa.

11.0 MAPUNGUFU YALIYOJITOKEZA KATIKA MASUALA YA NIDHAMU

Kutokana na ukaguzi uliofanyika katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na rufaa zilizowasilishwa, Tume imebaini upungufu ufuatao:-

- Mamlaka za Nidhamu kutofuata kanuni ambazo zinaitaka mamlaka husika kuanzisha mashtaka ya nidhamu na kusaini hati za mashtaka na barua za adhabu.
- Mamlaka ya Nidhamu kutowapatia nafasi ya kujitetea watumishi waliokuwa wakikabiliwa na mashauri ya nidhamu.
- Baadhi ya Mamlaka za Nidhamu kuwafungulia watumishi mashtaka ya nidhamu kwa makosa yale yale ambayo Mahakama iliwaachia huru ambapo ni kinyume cha Sheria.
- Kukosekana kwa hati za mashtaka wakati wa uanzishwaji wa mashtaka ya nidhamu au kutoteuliwa kwa Kamati za Uchunguzi.
- Hati za Mashtaka kutokuonyesha bayana kosa lililotendwa na mtumishi mtuhumiwa.

12.0 MAMLAKA ZA RUFAA

Kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, sehemu VI imeainisha Mamlaka za Rufaa katika Utumishi wa Umma kama ifuatavyo:-

- Kwa watumishi wa Umma ambao mamlaka yao ya Nidhamu ni Katibu Mkuu Kiongozi, Mamlaka ya Rufaa ni Rais;

- Kwa watumishi wa umma ambao mamlaka zao za Nidhamu ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, Watendaji Wakuu, na Mamlaka ya Serikali za Mitaa Mamlaka zao za Rufaa ni Tume ya Utumishi wa Umma;

- Mtumishi au Mamlaka ya Nidhamu ambayo haitaridhika na uamuzi ulitolewa na mamlaka yake ya Rufaa anayo haki ya kukata Rufaa kwa Rais ambaye uamuzi wake ni wa mwisho.

- Kwa upande wa walimu, mamlaka za Rufaa ni Kamati za Wilaya, Mkoa na Idara ya Utumishi wa Walimu, Tume ya Utumishi wa Umma na Rais.

13.0 HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA TUME KUKABILIANA NA UPUNGUFU KATIKA MASUALA YA AJIRA NA NIDHAMU

Kutokana na upungufu uliojitokeza, Tume ilichukua hatua zifuatazo:-

- Kuainisha maeneo yenye utata na migongano katika utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na Taratibu za Uendeshaji za Mwaka 2003 na kuyapeleka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili sheria iweze kurekebishwa.
- Kubatilisha matokeo ya usaili pale ambapo taratibu zilikiukwa na kuagiza zoezi hilo lifanyike upya kwa kufuata taratibu.
- Kufanya uchunguzi kuhusu ukiukwaji wa taratibu za ajira na nidhamu.

- Kutoa mafunzo na kusambaza miongozo kwa Mamlaka za Ajira na Nidhamu pamoja na Waajiri ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa urahisi kwa mujibu wa sheria.
- Kutoa maelekezo kwa njia ya Waraka kuhusu Uzingatiaji wa Sheria na Kanuni katika kushughulikia Masuala ya Ajira na Nidhamu. Imesisitizwa kwamba Mamlaka ya Nidhamu ndizo zinapaswa kuanzisha mashtaka na kutoa adhabu.
- Kutoa ushauri na maelekezo kwa Kamati na Bodi za Ajira kuhusu taratibu za kufuatwa wakati wa vikao vya usaili.

14.0 CHANGAMOTO

Katika kutekeleza majukumu yake, Tume inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Kuwepo kwa Mamlaka za Ajira na Nidhamu zinazotekeleza majukumu yao bila kuzingatia Sheria, Haki, Usawa na Uwazi.
- Kuhakikisha kuwa Taratibu za Uendeshaji zilizotajwa kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma zinakamilika na kuanza kutumiwa na mamlaka za Ajira na Nidhamu pamoja na Waajiri.
- Kuhakikisha kuwa Watendaji Wakuu katika usimamizi wa nidhamu wanawajibika na usimamizi thabiti wa utumishi wa umma kwa madhumuni ya kuleta ufanisi na tija.

- Kuhakikisha kuwa watumishi na watendaji wakuu katika utumishi wa umma wanabadilika kimtazamo katika utendaji kazi ili kuendana na matakwa ya Sheria ya utumishi wa umma.
- Kuwa na Rasilimali watu wa kutosha na wenye ujuzi, pamoja na vitendea kazi kama vile kompyuta, magari na samani za ofisi kwa ajili ya kufanya ukaguzi na tathmini.
- Kuhakikisha kwamba watumishi wa Tume wanapatiwa mafunzo ya kutosha ili kuweza kumudu majukumu yao.
- Kuziwezesha Mamlaka za Nidhamu na Ajira pamoja na watumishi kwa kuzipatia maelekezo na kutoa miongozo itakayowasaidia kuwa na tafsiri sahihi na inayofanana katika utekelezaji wa majukumu yao.

15.0 MATARAJIO YA TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Tume ina matarajio kwa watumishi wa umma na wadau kuwa watazingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya Tume katika kutekeleza majukumu yao.

Tume kwa upande wake inatarajia kufanya yafuatayo:-

- Kuimarisha ukaguzi katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutumia Mwongozo wa Ukaguzi utakaotolewa na Tume.
- Kuwawezesha watumishi wake ili kuweza kumudu vema majukumu yao.
- Kuhakikisha kuwa Taratibu za uendeshaji kwa kila kundi la utumishi ziwe zimekamilika na kuanza kutumika mapema ipasavyo.

- Kuhakikisha Mfumo wa Uboreshaji wa Utendaji Kazi Serikalini unakamilika katika Wizara, Idara zinazojitegemea,Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zote za Serikali ili kuleta tija,uwajibikaji na uboreshaji wa utoaji huduma.
- Kuhakikisha kuwa watumishi wanafanya kazi zao kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma.
- Kupata ushirikiano toka kwa Mamlaka za Ajira na Nidhamu pamoja na watumishi wa umma katika kuboresha Utumishi wa Umma.

16.0 HITIMISHO

Tume ya Utumishi wa Umma imejizatiti kutoa huduma kwa watumishi wa umma na Mamlaka za Ajira na Nidhamu kwa misingi ya haki, usawa na uwazi kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za Uendeshaji katika Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Ni matumaini ya Tume kwamba, watumishi na mamlaka hizo zitatekeleza wajibu wao kwa misingi ya sheria katika utoaji huduma bora kwa wananchi kwa ufanisi na kwa viwango vya juu ili kuleta maendeleo ya nchi yanayoendeleza hali ya maisha, kuondoa umasikini na kuongeza ustawi wa jamii hivyo kuufanya Utumishi wa Umma kutukuka.

SHERIA YA UTUMISHI WA UMMA NA.8 YA MWAKA 2002 NA MAJUKUMU YA TUME YA UTUMISHI WA UMMA:

YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI …….. …….. 1

2.0 MUUNDO WA TUME……..2

3.0 MADHUMUNI YA KUUNDWA KWA TUME……2-3

4.0 MAJUKUMU YA TUME YA UTUMISHI WA UMMA……..4-5

5.0 MAMLAKA ZA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA……...5-7

6.0 UTEKELEZAJI WA MASUALA YA AJIRA ……..7-10

7.0 MAMLAKA YA TUME KWA MAMLAKA MBALIMBALI ZA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA……10-12

8.0 MAPUNGUFU YALIYOJITOKEZA KATIKA MCHAKATO WA KUSHUGHULIKIA AJIRA.....11

9.0 MAMLAKA ZA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA UMMA……..12-13

10.0 MAMLAKA YA TUME KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA UMMA……...13-14

11.0 MAPUNGUFU YALIYOJITOKEZA KATIKA MASUALA YA NIDHAMU……..14-15

12.0 MAMLAKA ZA RUFAA……...15

13.0 HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA TUME KUKABILIANA NA UPUNGUFU KATIKA MASUALA YA AJIRA NA NIDHAMU……...16

14.0 CHANGAMOTO ……..17

15.0 MATARAJIO YA TUME YA UTUMISHI WA UMMA…….....18

16.0 HITIMISHO……..19